SUNNAH COLLEGE
MahadSunnah.com

# MŪSA ﷺ: KALEEMULLAAH

## (ALIYEZUNGUMZA NA ALLAH MOJA KWA MOJA)

IMEPITIWA NA KAMATI YA CHUO CHA SUNNAH ,
CHINI YA USIMAMIZI WA :


**SHEIKH DR. HAYTHAM SARHAAN**
(MWALIMU KATIKA MSIKITI WA MTUME ﷺ)


**SARHAAN.COM**

# MŪSA ﷺ: KALEEMULLAAH

## Jina.

Musa – na maana yake: mwenye ametolewa katika maji.
Jina ya baba yake: Imraan – na ni katika ukoo ya Ya'qūb ibn Iṣḥaaq ibn Ibrahim .

## Jina la kaka yake.

Harūn – alitumwa baada ya Musa kumsaidia ili kupata ushindi, na hii ilikuwa baada ya Musa kufanyia Harun shafa' kwa Allah. Yūsuf alikuwa ameingiza bani Israel –na ni yaqub- misr. Baada ya Yusuf kukufa, familia ya firaun wakawapatia adhabu kali. Allah akatuma Musa na Harun kwa bani Israel na firaun. Halafu akawatuma baada ya hao Daud na Suleiman kama vile imetajwa katika Quran.

## Jina la mtumishi wake.

Yusha' ibn nun – na alikuwa mtume baada ya Musa na Harun kukufa.

## Jina ya Mwalimu wake.

Al-khidr – Kuna tofauti baina ya ulamaa kama yeye ni mtume au ni mtu muadilifu.

## Jina la utani na sifa za kipekee.

"Kaleemullaah", Allah amempa fadla ambayo hajapatia mtu yoyote wakati Allah Alimuongelesha katika ardi kwa hikma ambayo Allah peke yake anajua. Kwa ajili ya hiyo ndo Musa ameitwa Kaleemullaah , Allah alimkarimisha na kumuongelesha kutoka juu ya mbingu ya saba bila ya kukua baina Yeye na Musa

wahyi au malaika kama ilivyokuwa na mitume na manabi wengine. Na ni miongoni mwa mitume watano wakubwa na aliyechaguliwa (naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.) Quran 33:69

yaani ako na cheo mbele ya Mola yake. Hassan Al-basri (Allah amrehemu) amesema dua yake ilikuwa inakubalika . Na Allah alimteua kwa ajili ya nafsi yake. (Kisha ukaja kama ilivyo kadiriwa, ewe Musa! Na nimekuteuwa kwa ajili ya nafsi yangu.) Quran 20:40,41

### Jina ya adui wake.

Fira'un (Anajulikana kama Ramsees wa pili kulingana na wanahistoria), waziri wake mkuu ni Haman vile Allah amesema katika Qur'an ﴿…Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao ...﴾ (Quran, 28:8)

### Jina ya kitabu chake.

Taurah na Suhuf – Kuna khilaf baina ya wanazuoni kama ni vitabu viwili au jina mbili za kitabu moja.

### Kuzaliwa na kifo.

Alizaliwa misri na akafa At-tur.

### Kazi yake.

Alikuwa akichunga kondoo.

### Jina la mlezi wake.

Aasiya – alikuwa bibi ya Fir'aun.

### Miujiza.

Yeye ni mtume aliyekuwa ni miujia mingi baada ya mtume Muhammad صلى الله عليه وسلم

### Mahala pake.

Ako katika mbingu wa sita kama ilivyokuja katika hadith ya Anas iliyokuwa katika Bukhari na Muslim.

### Fimbo yake.

Alikuwa akibeba fimbo na hii tunapata katika ayah ya Allah katika Qur'an.....(Akasema: Hii ni fimbo yangu;naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu Tena inanifaa kwa matumizi mengine.) Quran 20:18

### Dini yake.

Musa hakukuja na dini ya uyahudi bali alikuja na dini ya uislamu katika ufahamu yake ambaye inaeleweka ambaye inamaanisha (kujisalimisha kwa Allah peke yake). Hi indo dini ya manabi wote kutoka Nuh aleihi salam mpaka mtume Muhammadﷺ. Allah amesema Kuhusu Ibrahim katika Qur'an : ﴿ Ibrāhīm hakuwa ni Myahudi wala Mnaswara, Lakini alikuwa mfuasi na mtiifu wa amri ya Mwenyezi Mungu, aliyejisalimisha Kwake, na hakuwa ni miongoni mwa washirikina.].﴾ (Quran, 3:67), na Allah Akasema kuhusu Musa: ﴿ Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.

."﴾ (Quran, 10:84), kwa hivo uyahudi ni dini ya uongo na ambaye imebadilishwa na ambaye inaenda kinyume na dini aliyoleta Musa , sababu wayahudi wanaitwa yehud, na wafuasi wanaitwa yahud ima kwa sababu ya hao kusema ﴿ Sisi tumerejea kwako .﴾ (Quran, 7:156), "huduna" yaani tumetubu au tumerudi au kwa sababu imenasabishwa kwa yahud mtoto mkubwa wa Ya'qub.

### Kisa yake pamoja na mama yake.

Kisa yake haijakuja kwa ukamilifu isipokuwa katika Suratul Qasas katika kauli ya Allah.﴿ Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapo mkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya miongoni mwa Mitume . Basi wakamwokota watu wa Firauni, aje kuwa adui kwao na huzuni. Hakika Firauni na Hamana na majeshi yao walikuwa wenye makosa. Na mkewe Firauni alisema: Atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako. Msimuuwe! Huenda akatufaa, au tumpange kuwa mwenetu. Wala wao hawakutambua .Na moyo wa mama yake Musa ukawa mtupu. Alikuwa karibu kumdhihirisha, ingeli kuwa hatukumtia nguvu moyo wake ili awe miongoni mwa Waumini. Naye akamwambia dada yake Musa: Mfuatie. Basi naye akawa anamuangalia kwa mbali bila ya wao kujua. Na tukamjaalia awakatae wanyonyeshaji wote tangu mwanzo, mpaka dada yake akasema: Je! Nikuonyesheni watu wa nyumba watakao mlea kwa ajili yenu, nao pia watakuwa wema kwake? Basi tukamrudisha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli, lakini wengi wao hawajui.﴾ (Quran, 28:7-13).

### Ayah zake.

Allah amesema katika Qur'an: ﴿Na kwa yakini tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. ﴾ (Quran, 17:101):

1. **Fimbo:** ﴿ Basi akaitupa fimbo yake, na mara ikawa nyoka dhaahiri .﴾ (Quran, 7:107)
2. **Mkono:** ﴿ Na akatoa mkono wake, mara ukawa mweupe kwa watazamao.﴾ (Quran, 7:108)
3. **Ulimi:** ﴿ Na ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu.﴾ (Quran, 20:27-28) Allah alikadaria akatoa shida iliyokuwa katika ulimi wake ili iwe ni ayah
4. **Njia katika bahari:** ﴿Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa .﴾ (Quran, 26:63)

**5. ~ 9. Mafuriko, nzige, chawa, chura, na damu:** ﴿ Basi tukawapelekea Mafuriko, na nzige, na chawa, na vyura, na damu, kuwa ni Ishara mbali mbali. Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu .﴾ (Quran, 7:133)

### Sifa yake.

Mtume ﷺ alimsifu akasema niliona usiku wa isra' kijana mrefu rangi ya kahawia na nywele laini ni kama alikuwa miongoni mwa watu wa kabila ya Shanua, imepokelewa na bukhari na Muslim. Na hizi ni sifa za aliyekuwa na nguvu kama ilivyoelezwa na mtoto wa kike wa mzee (baadaye akawa mke wa Musa), kama vile Allah amesema katika quran: ﴿ "Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu ."﴾ (Quran, 28:26). Na hakuna nabi katika Qur'an amesimuliwa kama kufikia utu uzima wa ukamilifu isipokuwa

## MŪSA ﷺ: KALEEMULLAAH

Musa, kama vile Allah anasema katika Qur'an: ﴿ Na Musa alipo fika utu-uzima baraabara, tulimpa akili na ilimu. Na hivi ndivyo tunavyo walipa walio wema ."﴾ (Quran, 28:14).

**Sifa yake.**

1. **Subra mingi:** "Allah amrehemu Musa aliudhiwa Zaidi ya hii akasubiri." Bukhari na Muslim
2. **Elimu Mingi:** "Hakika Musa hiyo siku wakati alikuwa akitoa khutba kwa watu wake akawaambia hakuna mtu katika ardi ambaye ako na elimu kuliko mimi"' (Imepokelewa na Ahmad)
3. **Kutegemea Allah:** ﴿ " Yaweza kuwa Mola wangu Mlezi akaniongoa njia iliyo sawa..".﴾ (Quran, 28:22)
4. **Nguvu katika akili na mwili na amanah:** ﴿ Ewe baba yetu! Muajiri huyu. Hakika mbora wa kumuajiri ni mwenye nguvu na muaminifu..﴾ (Quran, 28:26)
5. **Wazi wa kifua:** ﴿ (Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu .﴾ (Quran, 20:25)
6. **Ushujaa , ujasiri na kufanya wepesi kusaidia watu:** ﴿ Basi Musa akawanyweshea.﴾ (Quran, 28:24)
7. **Kutimiza ahadi:** ﴿Basi alipo timiza muda wake ..﴾ (Quran, 28:29)
8. **Kusaidia waliodhulumiwa:** kama vile katika kisa ya Musa kumsaidia aliyedhulumiwa, Quran, 28:15.
9. **Unyenyekevu, kukiri fadla ya wengine na kukuwa na hima kutafuta elimu:** ﴿ Musa akamwambia: Nikufuate ili unifunze katika ule uwongofu ulio funzwa wewe ?"﴾ (Quran, 18:66)
10. **Kukuwa na huja ya hali ya juu na mantiki katika daa'wah na pia kufanya daa'wah kwa kiwango.**

11. **Kurudi kwa Allah na kufanya tawbah:** ﴿ Akasema:" Mola wangu Mlezi! Hakika mimi nimejidhulumu nafsi yangu; basi nisamehe ".﴾ (Quran, 28:16)
12. **Kuomba usaidizi kutoka Allah na Kumuani na kutaraji nusra kutoka Allah:**﴿ Musa) akasema: "Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa ."﴾ (Quran, 26:62)
13. **Kukuwa na uhuruma:** ﴿ Basi waache Wana wa Israili watoke nasi, wala usiwaadhibu .﴾ (Quran, 20:47)
14. **Kukuwa na hasira wakati mpaka za Allah zinafukwa:** ﴿. Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na kusikitika﴾ (Quran, 20:86)
15. **Kufanya uamuzi wa haraka:** ﴿ Hapo Mūsā akautoka mji wa Fir'awn akiwa katika hali ya kuogopa.﴾ (Quran, 28:21)
16. **Kukuwa na nguvu kuongea ukweli:** ﴿ Na hakika mimi bila ya shaka nakuona wewe, Firauni, kuwa umekwisha angamia . ﴾(Quran, 17:102)
17. **Kujua qadri ya wajibu wake:** ﴿ Na nipe waziri katika watu wangu, Harun, ndugu yangu. Kwake yeye niongeze nguvu zangu.﴾ (Quran, 20:29-31)
18. **Kutotaka dunya na kuchagua akhira:** ﴿ Mola wangu Mlezi! Hakika mimi ni mhitaji wa kheri utakayo niteremshia..﴾ (Quran, 28:24)
19. **Kukubali nasiha:** ﴿ Ewe Musa! Wakubwa wanashauriana kukuuwa. Basi toka! Hakika mimi ni katika wanao kupa nasaha. .﴾ (Quran, 28:20)
20. **Kukuwa na haya ya hali ya juu:** " Hakika Musa alikuwa ni mtu wa tabia njema na haya , hakuna kitu katika mwili yake

ilionekana kutokamana na haya aliyokuwa nayo." Bukhari na Muslim.

**Sifa maalum ya ummah wake.**

1. **Musa alitumwa kwa ummah miwil**: ummah ya watu wa fir'an, na ummah ya bani israil baada ya kuangamizwa kwa firaun.
2. **Ni mtume wa mwisho ambayo Allah aliangamiza ummah yao.** Kama vile Allah amesema katika Qur'an: ﴾ Na hakika bila ya shaka tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo,﴿ (Quran, 28:43) ibn Kathir amesema kwa tafseer yaani baada ya Allah kuteremsha taurah ummah haukuangamizwa wote mara moja.
3. **Akona wafuasi wengi baada ya mtume Muhammad ﷺ..** mtume Muhammad ﷺ alisema , "Ummah kubwa ilionyeshwa mbele yangu katika jannah nikauliza ni nani hawa Jibril? Akasema hawa ni wafuasi wa Musa."' Bukhari na Muslim.

**Alitulizwa na:**

Allah anasema katika Qur'an: ﴾watu wake walimkanusha Mūsā..﴿ (Quran, 22:44)

**Kuthibitishwa kutokuwa na hatia.**

Allah anasema katika Qur'an: ﴾Enyi mlio amini! Msiwe kama wale walio mtaabisha Musa, lakini Mwenyezi Mungu akamtakasa na waliyo yasema, naye alikuwa mwenye hishima mbele ya Mwenyezi Mungu.﴿ (Quran, 33:69)

**Kisa ya Musa katika Qur'an.**

Yeye ni nabi mwenye ametajwa sana katika Qur'an, ametajwa mara 136 na katika surah 34 tofauti, na surah ambazo ametajwa

sana ni Surat Al-A'raaf ( mara 21 ), Surat Al-Qasas ( mara 18), and Surat Ta-Ha ( mara 17 ). Sababu ya yeye kutajwa kwa wingi ni kwa sababu ya nguvu ya huja yake na ayah mingi aliyopatiwa, na kiburi kubwa aliyokuwa nayo fir'aun na kuvuka mpaka . Ibn S'di, (Allah amrehemu) amesema katika tafseer yake ukurasa ( 453): "Sana sana Allah analinganisha nubuwa wa Muhammad ﷺ na nubuwa wa Musa ﷺ, na baina vitabu zao na sharia zao kwa sababu vitabu zao ni vitabu bora na sheria zao ni sheria ziliokuwa na ukamilifu Zaidi na nubuwa zao ni daraja ya juu na wafuasi wao ni wengi sana."

### Ndoa yake.

Musa ﷺ alitumia miaka kumi wa umri wake sharifu kwa kutumikia mtoto wa kike wa Shuab. Allah amesema: ﴿ "Akasema: Mimi nataka kukuoza mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane. Ukitimiza kumi, khiari yako." ﴾ (Quran, 28:27) Ibn ul-Jawzi,(Allah amrehemu), amesema katika "Sayd u-Khaatir" ukurasa( 40): "Kama ndoa haingekuwa miongoni mwa vitu bora, maisha mingi ya ma nabi wengi haingetumika ndani yake."

### Kisa yake katika Qur'an kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

1. Mama yake kumueka katika bahari wakati akiwa mchanga, kuokolewa kwake, yeye kuingia ikulu ya fir'aun.
2. Yeye kukuwa kijana baro baro, yeye kuua kijana miongoni mwa watu wa fir'aun, kutoroka kwake akielekea misri.
3. Kukutana kwake ambaye ilikuwa na Baraka katika madyan.
4. Kutimiza kwa ahadi yake na yeye kurudi Misr.

5. Kukuja kwake kwa mlima alipoongea na Allah.
6. Kukutana na fir'aun.
7. Kisa yake na waganga na kuondoka kwake na bani Israel kutoka Misr.
8. Kukutana kwake na mja mwema, Al-Khidr.
9. Kisa yake na Saamiri na watu wake kuabudu ndama.
10. Kisa yake na Qarun .
11. Kisa yake na ng'ombe.(Al-Baqarah).

**Kisa ya ajabu.**

Mtume ﷺ amesema, "Je mumeshindwa kukuwa kama ajuza wa bani isarel?" Wakauliza, "Ewe Mtume ﷺ, kisa yake ilikuwa aje?" akasema, "Wakati Musa alitoka Misr na bani isarel walipotea njia. Musa akauliza, 'Hii ni nini?' wanachuoni wao wakasema, 'Hakika wakati Yusuf ﷺ alikaribia kufa , alichukua ahadi kutoka sisi ya kuwa tusitoke Misr mpaka tuchukue mifupa yake nasi.' Musa akauliza , 'Nani anajua mahali ya kaburi yake?' wakasema ajuza mmoja wa bani israel, akaletwa. Musa akasema , 'Nionyeshe kaburi ya Yusuf ﷺ.' Akasema mpaka unipatie kitu nitakachokuambia, Musa akasema , 'Nini hiyo?' Akasema, 'nataka niwe nawe katika jannah.' Musa alichukia kumkubalia akaomba Allah amuongoze. Allah alipatia wahyi Musa ya kuwa akubali alichokiomba huyo ajuza. Baada ya hayo akawapeleka mahali kuna maji kidogo akasema, 'limeni hapa,' wakalima na wakapata mifupa ya Yusuf ﷺ. Wakati waliitoa wakaonyeshwa njia ambaye ilikuwa na mwangaza." (Imepokelewa na Ibn Hibbaan na Al-Haakim, na imesahihishwa na Al-Albaani)